



Mercy Housing

Karibu
Nyumbani Kwako
Mahali Papyrus

Maelezo

<i>Picha zilizoko kwenye kitabu hiki na maana zake</i>	<i>i</i>
<i>Vitu vya kawaida na majina yake</i>	<i>ii</i>
<i>Kulipa bili</i>	<i>1</i>
Namna Ya Kutunza Nyumba Ya Kukodisha	
<i>Ukaguzi unao fanyika kabla ya kuhama</i>	<i>2</i>
<i>Chumba cha kukaribisha wageni</i>	<i>3-5</i>
<i>Wadudu wa kitandani (kama vile kunguni)</i>	<i>6</i>
<i>Jikoni</i>	
<i>Maandalizi ya chakula</i>	<i>7</i>
<i>Usafishaji wa vyakula vilivyomwagika</i>	<i>8</i>
<i>Upikaji na Ukandaji</i>	<i>9-10</i>
<i>Mashine ya kuosha vyombo vya kulia chakula</i>	<i>11</i>
<i>Jiko la umeme</i>	<i>12</i>
<i>Sinki/mashine ya kuondoa uchafu wa chakula</i>	
<i>kwenye sinki</i>	<i>13</i>
<i>Takataka/pipa la takataka</i>	<i>14</i>
<i>Chumba ca kuoga</i>	
<i>Usafi kwa ujumla</i>	<i>15</i>
<i>Shida mbalimbali za chooni</i>	<i>16</i>
<i>Kuvuja na kumwagika kwa maji</i>	<i>17</i>
<i>Ufuaji nguo</i>	<i>18</i>
Usalama Na Ulinzi	
<i>King'ora cha moshi</i>	<i>19</i>
<i>Moto</i>	<i>20-22</i>

Usalama Na Ulinzi

<i>Njia za ndani ya jengo</i>	<i>23</i>
<i>Chekecheke za mlango na madirisha</i>	<i>24</i>
<i>Tahadhari ya Afya</i>	<i>25</i>
<i>Uvutaji sigara</i>	<i>26</i>
<i>Vibanio vya milango, funguo, Watu usiowafahamu</i>	<i>27-28</i>

Barua Na Matangazo

<i>Barua na matangazo yaliyobandikwa</i>	<i>29</i>
<i>Maombi ya utengenezaji wa vitu</i>	<i>30</i>

Ujirani Mwema

<i>Kelele, kusuluhisha mizozo, wanyama wa nyumbani</i>	<i>31</i>
--	-----------

Matumizi Bora Ya Umeme

<i>Kipima joto cha nyumba</i>	<i>32</i>
<i>Vitu vya kukusaidia</i>	<i>33-34</i>

Kwakifupi

Kitabu hiki kimeandaliwa kutumika kama sehemu ya ufahamishaji inayomhusu meneja wa kesi ya wakimbizi na familia ya wakimbizi. Hakikuandikwa kama kifungu kinachoweza kusimama pekee kwa nia hii ya kuwaelekeza wakimbizi.

Kitabu hiki kimeandikwa kwa ushikiano kati ya African Community Center in Denver, Colorado na Mercy Housing, Inc.

Vielekezo na michoro ya metolewa na Carol Kimball.

The Africa Community Center ni ofisi ya utendaji ya Jamii ya Maendeleo ya Waethiopia (ECDE) yenye makao yake makuu Arlington, VA.

Andiko hili limetolewa na Technical Assistance for Refugee Housing Services project, Fungu #90RB0023. Mercy Housing, Inc., ilitunukiwa fungu hili na Ofisi ya Kuwapatia Makao Wakimbizi (ORR), Wizara ya Afya na Huduma za Watu ya Marekani. Maoni yaliyotolewa kwenye andiko hili sio lazima yakubaliane na maoni ya ORR.

Katika matumizi ya kitabu hiki, utaona picha mbalimbali kwenye kurasa maalum – ifuatayo ni maana ya picha hizi:



Picha hii inamwonyesha meneja wako anayekuhudumia. Huyu ndiye mtu atakaye kuonyesha kurasa mbalimbali kwenye kitabu hiki.

Jina: _____

Namba ya simu: _____



Hii ina maanisha meneja wa majumba ya kukodisha unamoishi.

Jina: _____

Namba ya simu: _____



Huduma za afya Zimamoto Polisi

Kuita 9-1-1 kwa kutumia simu yako ni njia ya kupata msaada haraka na mapema iwezekanavyo unavyokuwa na dharura. Tumia simu hii endapo una dharura tu.




Hii picha inamaanisha “**HAPANA**” Usifanye kitendo kinachoonyeshwa kwenye picha hii.



Picha hii inamaanisha kwamba unapoteza pesa zako bure.

Usijaribu kufanya vitendo hivi.



Fanya hivi kila siku.




Fanya hivi mara moja kwa wiki.




Fanya hivi mara moja kwa mwezi.


Vitu vya kila siku na majina yake




Tangazo la
kufukuzwa
kwenye nyumba
ya kukodisha




Friji



Sinki
Vifungulio vya
bomba ya maji




Cupa la kuzima
moto




Takataka
Machine ya
kuondoa
uchafu wa
chakula
kwenye sinki



Sehemu ya
kuogea
Mtungi wa
sehemu ya
kuogea



King'ora cha
moshi



Jiko la umeme
Umbali




Choo



Pipa la takataka
Taka
Takataka




Mashine ya kuosha
vyombo



Kipima joto
cha chumbani
au themostati



Machine ya kufulia
nguo



Mawasiliano kwa spika



Mashine ya
kubadilisha hewa
ilioko dirishani
Mashine ya
kubadilisha hewa

Kulipa bili



Unalazimika kulipia nyumba, bili ya maji, umeme, na bili zingine zote kwa kipindi kinachotakiwa ***KILA MWEZI*** ili kulinda rekodi zako za malipo. Rekodi nzuri za kuonyesha ulipaji wako wa bili mbalimbali kwa tarehe inayotakiwa itakusaidia unapotaka kukopa pesa kununua nyumba, gari, au kujilipia chuo cha elimu. Tafadhali tengeneza orodha itakayo kusaidia kukumbuka kulipia bili zako kwa terahe zinazotakiwa.


KAMWE USITUME PESA TASLIMU KWENYE BARUA!



Namna Ya Kutunza Nyumba Ya Kukodisha

Ukaguzi unao fanyika kabla ya kuhama

Wewe na menaja anayekusaidia pamoja na meneja wa nyumba ya kukodisha lazima mtazame kila chumba kwenye nyumba unayokodisha ili kuhakikisha kwamba hakuna vitu vilivyo vunjika au vinavyohitaji matengenezo kabla ujahamia kwenye nyumba hiyo. Hii itakusaidia kurudishiwa pesa za amana wakati utakapoamua kuhamia mahali pengine.



January						
S	M	T	W	T	F	S
			1	2	3	4
5	6	7	8	9	10	11
12	13	14	15	16	17	18
19	20	21	22	23	24	25
26	27	28	29	30	31	

Safisha mkeka wa ndani kwa kutumia mashine ya kusafisha angalau mara moja kwa wiki. Kama kitu chochote cha majimaji kikimwagikia kwenye mkeka wa ndani, safisha kwa kutumia sabuni na maji mara tu baada ya tukio hilo. Sakafu ya mbao lazima ifagiliwe kila wiki.

Viti na vitu vigne vinavyohusiana na sebule ambavyo ulivileta kwenye nyumba ya kukodisha ulipoingia, isipokuwa vifaa vyote vilivyokuwemo ulipohamia, ni mali yako. Meneja wa jumba la kukodisha atatazamia kwamba utachukua vitu vyote vilivyo vyako utakapo hama. Kama una maswali kuhusu vitu ambavyo unaweza kuchukua utakapohama, soma karatasi za makubaliano au muulize meneja anayekusaidia.

Vua viatu uingiapo nyumbani. Hii itakusaidia kuweka mkeka wa ndani katika hali ya usafi.





Usimwage kitu chochote cha majimaji kwenye mkeka wa ndani. Hii itasababisha doa ambalo ni vigumu kulisafisha.



Safisha ***MARA MOJA*** endapo kitu chochote kitamwagika kwenye mkeka wa ndani.



**KAMWE USITUMIE
KIONDOA MADOA KWENYE
NGUO KUSAFISHA MKEKA
WA NDANI!**



Kama kuna doa ambalo umeshindwa kusafisha muulize maneja anayekusaidia au meneja wa majumba wakushauri namna ya kulisafisha.



Kwa madoa ambayo ni makubwa yasiyosafishika, unaweza kukodisha mashine ya kusafisha mkeka kwenye stoo unamonunua vyakula.



Wafundishe watoto wako WASICHEZEE mapazia na pia WASIANDIKE kwenye kuta.

Wafundishe watoto wako kutumia vitu vyote kwenye nyumba ya kukodi kwa uangalifu sana.

USIWARUHUSU warukeruke kwenye viti.



Wadudu wa vitandani (Kunguni)



Ukiumwa na wadudu wa kitandani ngozi yako hubadilika kwa kuvimba na kuwa nyekundu.



Wadudu wa kitandani huishi kwenye mikunjo ya nguo, kwenye kona za kuta, kwenye mkeka, na kwenye matandiko.

Kama ukigundua kwamba kuna hawa wadudu kwenye kitanda, fua shuka na nguo zote zinazohusiana na kitanda kwa maji moto na sabuni na kuzikausha kwenye machine ya kukausha nguo kwa joto la juu. Tumia mashine ya kufagia mkeka wa ndani kuvuta uchafu wote kwenye godoro, viti, mkeka, na kona za kuta na ondola mfuko wa uchafu kwenye machine mara umalizapo na kuupeleka kwenye pipa la takataka.



KAMWE USIOKOTE VITI, VITANDA, AU VITU VYOVOYOTE KUTOKA MITAANI NA KUVILETA NDANI!



Sogeza vitanda na makochi mbali na kuta.

Usiache shuka ziguse sakafu.

Weka miguu ya vitanda na viti kwenye makopo yenye sabuni ya maji.

Utayarishaji wa Chakula



Kama ukiharibu maeneo haya ya mbao, itabidi ulipe.



**KAMWE USIWEKE SUFURIA YA MOTO
JUU YA MAENEO YA MBAO YA JIKONI**

Tumia kitambaa kizito cha jikoni au kitambaa cha kawaida chini ya sufuria ya moto




**KAMWE USIKATIE KITU
CHOCHOTE KWENYE MAENEO
YA MBAO YA JIKONI**



**KAMWE USIKATIE KITU
CHOCHOTE KWENYE SAKAFU**



Usafishaji wa masazo ya vyakula



Safisha jiko na maeneo ya mbao kila siku.



Kamwe usiache chakula nje kwenye maeneo ya jiko bila kukifunika vizuri. Kutokufunika chakula kutawavutia wadudu na panya.

WADUDU WAKISHAINGIA NYUMBANI KWAKO ITABIDI KUWALIPA WATU WA IDARA YA KUUA WADUDU KUWAONDOA.



Ni bora kufunika chakula na kukiweka kwenye friji. Safisha friji mara kwa mara kwakutumia maji na sabuni.

UTAKAPO HAMA, ITABIDI ULIPE KAMA FRIJI YAKO HAIKO KATIKA HALI YA USAFI!



Kupika na Kukanda


Unapopika chakula kwenye stovu, kila mara anza na moto wa kiasi. Ukianza na moto mkali, unaweza kuunguza chakula na kuharibu sufuria. Kwa kutumia moto mkali unaweza pia kuyeyusha kabisa sehemu ya chini ya sufuria.



Tumia kitambaa kizito unapoepua sufuria ya moto na vitu vingine vyovyote ambavyo vimetumika kwenye jiko la moto au oveni.

**JIKO LILILOWASHWA NA OVENI YA MOTO
VINAWENZA KUKUCHOMA VIBAYA SANA!**


Kupika na Kukanda



Kutumia jiko la oveni kukanda vitu kama vile mkate, tumia kipimo cha moto cha digirii 350, au fuata maelezo yaliyofafanuliwa kwenye mdumu la chakula unachopika.

Kuwasha oveni kwa kutumia kipimo cha moto wa juu kwenye kiwashio kutasababisha chakula unachopika kuungua.

Safisha mmwagiko wowote wa chakula kwenye oveni na juu ya jiko mara tu jiko litakapo poa.



USICHOME AU KUPIKA KITU CHOCHOTE JUU YA JIKO BILA YA KUTUMIA SUFURIA!

Mashine yakuosha vyombo

Mashine ya kuosha vyombo hua wadudu kwenye vyombo vichafu. Haisugui vyombo au ifanye kazi ya mashine yakuondoa uchafu.


Kila wakati sugua na pangusa mabaki ya chakula kwenye kipipa cha ndani cha takataka na suuza vyombo kabla ya kuviweka kwenye mashine ya kusafisha vyombo.

Mashine ya kusafisha vyombo hutumia sabuni maalum. Sabuni hii ni nzito na ina nguvu sana kwahiyu usijaze kipimo kinachotakiwa kupita kiasi. Usitumie sabuni ya kawaida au sabuni ya kufulia nguo kwenye mashine hii.

Fagia sakafu kila siku na deki kwa maji na sabuni kila wiki.



Jiko la umeme la kupikia



Pangusa na safisha mabaki ya vyakula na mafuta yaliyomwagika **HARAKA SANA**, na safisha jiko la kupikia kila siku.



Usimwage mafuta kwenye sinki. Yahifadhi kwenye kopo na yatupe kwenye pipa la takataka.



Chakula kilichomwagika au kuungua juu ya jiko na mafuta ni hatari. Vina harufu mbaya na huvutia wadudu na panya.

MAFUTA YAKIMWAGIKA YANATELEZA NA YANAWENZA KUSABABISHA KUANGUKA VIBAYA SANA!

MAFUTA YALIYOMWAGIKA YANAWENZA KUSABABISHA MOTO!

Sinki na Mashine ya kuondoa Uchafu kwenye sinki



Inawezekana nyumba ya kupangisha unayoishi inasehemu yenye mashine kubwa ya kusaga takataka hizi.

Kila unapotumia machine hii ya takataka fungua bomba ya maji baridi. Usiwashe mashine hii kabla ya kufungua maji baridi.

Usiweke mifupa, makasha ya mayai, vifundu vya matunda, maganda ya vitunguu, seleri, au chuma cha aina yoyote kwenye mashine hii ya uchafu.



Kama mashine ya kuondoa uchafu kwenye sinki imekwama, maji yanaweza yasimame na yasiende popote. Zima machine hiyo na mjulishe mara moja meneja wa nyumba ya kukodi.

KAMWE USIINGIZE MKONO KWENYE SINKI LENYE MASHINE HII YA UCHAFU.

Pipa la takataka

January						
S	M	T	W	T	F	S
1	2	3	4	5	6	7
8	9	10	11	12	13	14
15	16	17	18	19	20	21
22	23	24	25	26	27	28
29	30	31				

Weka uchafu kwenye vipipa vilivyotolewa kwenye nyumba yako unamoishi. Kabla ya kuweka uchafu kwenye vipipa hivi, hakikisha umeweka mfuko wa nailoni wakushika na kubebea uchafu.

Toa takataka nje mara kwa mara na kuipereka kwenye pipa kubwa la takataka liloko nje. Harufu ya takataka huvutia wadudu na panya na husababisha malalamiko kwa meneja wa majumba kutoka kwa majirani.

KAMWE usiache takataka nje ya mlango au kwenye njia za ndani ya jengo.



Kama eneo unaloishi wana programu ya kutenga uchafu kwa ajili ya utunzaji wa mazingira, fuata maelezo ya kutenganisha vile vitu ambavyo vinafaa kutupwa kwa uangalifu ili kulinda mazingira.



Usafi kwa Ujumla

January						
S	M	T	W	T	F	S
		1	2	3	4	
5	6	7	8	9	10	11
12	13	14	15	16	17	18
19	20	21	22	23	24	25
26	27	28	29	30	31	

Maliwato lazima isafishwe kila wiki. Hii ni pamoja na sakafu, nje na ndani ya choo, sinki, na sehemu ya kuogea.

Usiruhusu nywele kuingia kwenye sehemu inayotoa maji nje aitha kwenye sinki au sehemu ya kuogea.



Matatizo ya Choo

January						
S	M	T	W	T	F	S
			1	2	3	4
5	6	7	8	9	10	11
12	13	14	15	16	17	18
19	20	21	22	23	24	25
26	27	28	29	30	31	

Safisha nje na ndani ya choo na kuzunguka eneo lote kila wiki. Safisha mkojo kama ukianguka kwenye sakafu mara tu baada ya tukio hilo.

KAMA CHOO CHAKO KIKIZIBA NA KUSABABISHA MAJI KUJAA NA KUFURIKA CHOONI, MWARIFU MENEJA WA MAJUMBA MARA MOJA NA HARAKA IWEZEKANAVYO!



Tumia brashi kusafisha choo.

Kamwe usitupe vitu vyoyote vya usafi wa kike, takataka, chakula, karatasi za kusafishia jiko, karatasi kubwa kupita kiasi za chooni, au vitu vingine vyoyote visivyohusiana na choo kwenye choo.

FUNDISHA WATOTO WAKO KWAMBA NI MARUFUKU KUTUPA SANAMU ZAO ZA KUCHEZEA AU VITU VINGINE VYOVYOTE CHOONI.



USITUMIE BRASHI UNAYOTUMIA KUSAFISHA CHOO KWA KUSAFISHIA KITU KINGINE CHOCHOTE!

Uvujaji maji na Kumwagika

Hakikisha pazia la mahali pa kuogea limo upande wa ndani ya mahali pa kuogea wakati wote na kausha maji yaliyoanguka kwenye sakafu mara tu baada ya tukio hilo.

Mkeka wa nailoni usioteleza utazuia kuanguka kwenye eneo la sakafu ya kuogea.

KAMA MAJI YAMEZIBA AU YANAVUJA MUARIFU MENEJA WA MAJUMBA MARA MOJA NA HARAKA IWEZEKANAVYO!

Utatakiwa kulipa uaribifu utakaosababishwa na maji yanayovuja kwa kuto kutoa taarifa ya tukio hili haraka iwezekanavyo.



1. Tenganisha nguo kutegemeana na rangi kwa kutenganisha rangi nyeupe na rangi zingine.
2. Tumia kionyesho kwenye mashine kuchagua maji vuguvugu kwa kuosha na maji baridi kwa kusuuza, au fuata maelekezo yaliyo andikwa kwenye kola ya nguo inayoeleza namna ya kuosha aina ya nguo unayotaka kuosha.
3. Anzisha maji kwenye mashine, weka sabuni ya kuoshea, halafu weka nguo.
4. Usijaze machine ya kuoshea au kukaushia nguo kupita kiasi.
5. Kila mara ukaushapo nguo, safisha chekecheke inayoshika nyuzi na pamba zanguo zinapokauka ilioko kwenye mashine hiyo.
6. Usiache nguo zako kwenye eneo la kufulia nguo bila ya wewe kuwepo kwenye eneo hilo.



Meneja wa jumba unamoishi lazima ahakikishe kwamba nyumba yako ina king'ora cha moshi.

King'ora cha moshi lazima kiwe kinafanya kazi. Hii inaweza kukuponya maisha yako kama moto ukitokea kwenye nyumba yako kwa kupiga kelele kiguswapo na moshi.

KAMA VING'ORA VYAKO VYA MOSHI VINATUMIA BETIRI, HAKIKISHA KWAMBA BETIRI HIZO NI MPYA NA LAZIMA UBADILISHE BETIRI HIZO MARA MOJA KWA MWAKA. CHAGUA SIKU ILIYO MUHIMU KWAKO KATIKA MWAKA AMBAYO ITAKUKUMBUSHA KUBADILISHA BETIRI HIZI.



Jaribisha king'ora cha moshi kwa kubonyeza kiwashio kilichoko hapo mbele.

Kama king'ora cha moshi kikipiga kelele wakati unapopika chakula kwa ajili ya moshi, kizime kwa kutumia kiwashio hicho.



KAMWE USING'OE AU KUTUPA KINGORA CHA MOSHI!

Kama king'ora cha moshi kwenye nyumba yako hakifanyi kazi, mwarifu meneja wa majumba.

Unatakiwa ufahamu mahali vizima moto vilipo kwenye nyumba unamoishi, na jifunze vinavyotumika kuzima moto.



**KAMWE USITUMIE MAJI KUZIMA MOTO
ULIOSABABISHWA NA MAFUTA !**



- 1) Kama moto ni mdogo, jaribu kuuzima kwa kuufunika na sufuria nyingine au kifunikio.
- 2) Kama moto ni mkubwa, tumia kizimamoto kama ulivyooyeshwa.

Mara tu utumiapo kizimamoto, lazima umfahamishe meneja wa majumba ili akijaze kiwe tayari kwakutumika wakati mwingine unapokihitaji kuzima moto.

- 3) Kama unaona kwamba hauna uwezo wa kuzima moto unapotokea,

WAARIFU WATU WOTE WAONDOKE KWENYE JENGO NA PIGA SIMU YA AJALI YA 911 KUPATA MSAADA!

MAISHA YA WATU NI MUHIMU KULIKO VITU!





KAMA MOTO NI MKUBWA KUPITA KIASI, ITA NAMBA HII YA 911!

Kama unauwezo, kimbia nje mara moja. Inama chini au tambaa kukwepa moshi na jaribu kukwepa kupumua moshi huo. Waarifu majirani kama unauwezo.

KAMWE usitumie lifti kukimbia moto – teremka kwenye ghorofa kwa kutumia ngazi za kawaida kwenye jingo.



Kama mlango wako ni wa moto, usijaribu kuufungua. Tumia dirisha kama uko kwenye ghorofa ya kwanza, au tumia njia iliyotolewa ya kukimbia moto au subiri dirishani kwa msaada. Weka taulo zilizoloanishwa kwenye maji kando ya milango kuzuia moshi kuingia ndani, na tumia nguo zilizoloanishwa kupumua.





Njia za ndani ya jengo na sehemu zinazotumiwa na jumua ambazo hazijapangwa vizuri ni hatari na zinaweza kuwa mtego wakati wa tahadhari kama vile moto.



Kuweka maeneo haya ya jumua kwenye jengo lako katika hali ya usafi, utaratibu na kupangwa, pia husaidia kujenga ujirani mwema.



Milango na madirisha yenye chekecheke ni muhimu kuzuia watoto wadogo na wanyama wa ndani kukaa ndani, na pia kuzuia wadudu na wanyama wasiingie ndani.

Kama chekecheke hizi zikichanika au kama zimekwisha, mwarifu meneja wa majumba.





ITA NAMBA HII 911 KAMA KUNA MTU ANAYEUMWA VIBAYA!

Waokoaji/wasaidizi watakuja mapema iwezekanavyo kukusaidia. Wakisha gundua shida, watakusaidia kuamua kama utahitaji gari la msaada la hospitali (king'ora) kumpeleka mgonjwa hospitalini.

Katika kupata msaada huu kunavitu ambavyo unaweza kuwajibika kulipia.



Sigara za hapa Marekani huendelea kuwaka hata kama hauendelei kuzivuta.

Kwahiyo lazima kila mara uhakikishe kwamba umezizima sigara kabisa kabla ya kuzitupa.



Usivute sigara kitandani, au mahali popote ambapo upo kwenye hatari ya kulala usingizi.



Utalipia vitu vyovyote vitakavyokuwa na michomo ya sigara kwenye nyumba ya kukodisha.



Usivute sigara unapokuwa umekaa na watoto au wanawake wajawazito.



Watu wazima na watoto kamwe wasifungulie milango kwa njia yoyote watu usiowafahamu.



KAMA UKIONA WATU WAKIIBA, ITA 911!

Kila mara hakikisha umefunga na kubana milango, hata kama uko nyumbani. Kwa usalama wako, fungua na bana madirisha kabla ya kuondoka kwenda mahali popote.

Usiwafungulie watu usiowafahamu mlango na kuwaruhusu kuingia ndani ya jengo.



Kama ukisahau funguo ndani au ukijifungia nje ya nyumba yako ya kukodisha, itabidi ulipe \$50.00 au zaidi ili meneja wa majumba akufungulie mlango. Kama ukipoteza ufunguo wa nyumba yako malipo ni ya juu zaidi utakayolipa ili kuweka kitasa kipya.



Kama watu usiowafahamu wanataka kuingia waambie wakuonyeshe kitambulisho chao kabla ya kuwafungulia mlango hata kama wamevaa unifomu.





Soma barua zako na weka karatasi zako muhimu mahali pa usalama.

Kama kuna kitu chochote usichoelewa, muulize meneja wa kesi yako.



Cheki boksi lako la barua kila siku. Usitupe makaratasi ya barua usizozitaka ovyo ovyo kwenye eneo la kuingilia.



Kama tangazo limebandikwa kwenye mlango wako, lazima uzingatie kulisoma na kujibu **MARA MOJA!**

Matangazo kama haya ni njia moja ambayo inatumiwa kukutaarifu kufukuzwa kwenye jumba.



Mameneja wa majumba mara nyingi wanataka maombi ya kukarabati vitu vilivyoharibika yaletwe kwa njia ya maandishi kabla ya kukarabati vitu hivi. Tumia fomu ya kuomba marekebisho haya ya ukarabati, au muombe meneja wa kesi yako akusaidie.

Anwani hii ya k wenye mtandao www.refugeehouse.org ina fomu ambayo unaweza kutumia.



Choo changu kimeziba.



Mashine ya takataka ya sinki la jikoni haifanyi kazi.



Bomba ya maji inavuja



Jiko langu la kupikia halifanyi kazi.



Chekecheke ya mlango au dirisha inahitaji ukarabati.

Kwa kawaida watu wengi huenda kulala saa 4 usiku. Tafadhali hakikisha watoto wako hawapigi kelele, hakikisha mazungumzo yenu ni ya utaratibu bila kelele na usisikilize musiki kwa sauti kubwa kati ya saa 4 usiku na saa 2 asubuhi.

Ni lazima ufuata sheria zilizowekwa na meneja wa majumba kuhusu kelele. Sheria hizi zinapatikana kwenye makubaliano ya mkataba wako.



Kama ukigombana na jirani zako, jaribu kusuluhisha ugomvi huu pamoja. Kama ikishindikana, muombe meneja wa kesi yako au meneja wa majumba akusaidie kusuluhisha.




Baadhi ya nyumba za kukodisha uruhusu wakaaji kuwa na wanyama wa nyumbani kama mbwa au paka. Hakikisha unafahamu ni wanyama gani wanaruhusiwa kweneye nyumba hizi za kukodi.



Wapangishaji wa nyumba kwa kawaida ulipia nguvu zinazohusiana na kiongeza joto, umeme, na kibadilisha hewa. Vitu hivi vinaweza kuwa ghali sana. Fuata maagizo haya ili kupunguza gharama za malipo haya.

Themostati inatumika kupima na kupunguza au kuongeza joto kwenye nyumba yako ya kupangisha. Wakati wa baridi na barafu inatakiwa iwekwe kwenye kiwango cha digrii 65 au 75, na kati ya digrii 70 na 75 wakati wa joto na kiangazi.



Kuongeza joto zaidi ya kiwango hiki kilichotajwa haifanyi joto kutokea kwa haraka, na kama ukisahau kupunguza baada ya kuongeza kupita kiasi, itakubidi kulipa pesa nyingi sana.



WAKATI UMEWASHA THEMOSTATI KWA AJILI YA KUONGEZA JOTO AU BARIDI, HAKIKISHA KWAMBA MILANGO NA MADIRISHA YAMEFUNGWA.



Uondokapo kwenye nyumba yako kwenda mahali popote hakikisha umezima taa na redio. Acha taa moja tu au mbili zikiwaka ili kama mwizi anafikiri kuingia kuiba adhani kuwa kuna mtu nyumbani.



**KAMWE USIACHE MADIRISHA WAZI
WAKATI UMEWASHA THEMOSTATI KWA
AJILI YA KUONGEZA JOTO AU KUPOOZA
NYUMBA!**

Kama ukisikia hewa yabaridi inaingia ndani kwenye milango au madirisha yaliyofungwa, mweleze meneja wako wa majumba ili azibe maeneo yanayoruhusu baridi kuingia.



Uvaaji soksi, suruali, na nguo za mikono mirefu pamoja na makoti na nguo za ndani zitakusaidia kukwepa baridi na ni gharama ya chini ukilinganisha na kuongeza joto kutumia themostati.



**KAMWE USITUMIE JIKO LA KUPIKIA AU OVENI
KAMA MOTO WA KUOTA WALA USILIWASHE
KUONGEZA JOTO NDANI!**



Hakikisha milango ya friji imefungwa wakati wote. Kuacha milango hii wazi kunapoteza nguvu za umeme na kutasababisha chakula kilicho hifadhiwa humo kuharibika, na ukila chakula kilicho haribika utaugua.

Kwakifupi

- 1) Lipa bili zako
- 2) Hakikisha vitu vyote viko katika hali ya usafi.
- 3) Tunza mali zote
- 4) Fahamu taratibu za ajali za moto na ajali au dharura zingine.
- 5) Soma barua zako na matangazo yaliyobandikwa.
- 6) Jibidisha kuwa jirani mwema.
- 7) Usipoteze nguvu za umeme na joto bure.



Lipa bili zako.



Tunza mali zote.



Jibidisha kuwa jirani mwema.



Hakikisha vitu vyote viko katika hali ya usafi.



Fahamu taratibu za ajali za moto na ajali au dharura zingine.



Soma barua zako na matangazo yaliyobandikwa.



Usipoteze nguvu za umeme na joto bure.

Watendaji pamoja wa andiko hili:

Jennifer Gueddiche, Mkuu wa Office ya Jamii ya Africa; Scott Robbins Mkuu wa Kitengo cha Kuwapatia Majumba Wakimbizi cha Mercy Housing; na Carol Kimball, Mchoraji, na Zarawasaidizi Jennifer Harden na Zara Tenore.



Mercy Housing

1999 Broadway, Suite 1000, Denver, CO 80202
Phone: 303-830-3300 Fax: 303-830-3301
www.mercyhousing.org www.refugeehouse.org